TANGAZO LA SERIKALI NA. 206 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USHURU WA MADINI YA UJENZI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 412 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2024 ambazo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 5

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 5 kwa-
(a) kufuta aya (a); na
(b) kubadili mpangilio wa aya (b), (c) na (d) kuwa aya (a), (b) na (c) mtawalia.

Marekebisho ya kanuni ya 15

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 15 na kuiandika upya kama ifuatavyo;

"Kufifilisha kosa

15. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili na kulipa ushuru anaodaiwa."

Marekebisho ya Jedwali la Pili

4. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Pili-

(a) kwa kuongeza maneno "ya udongo" mara baada ya neno "Matofali" lililopo katika safu ya pili ya kipengele cha 6; na

(b) kwa kubadili mpangilio wa vipengele vya (5), (6), (5), (6), (7), (8) na (11) kuwa vipengele vya (5), (6), (7), (8), (9), (10) na (11), mtawalia.

Dodoma,
10 Januri, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*